**KAULI YA SERIKALI ITAKAYOTOLEWA NA WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) MHE. MHANDISI HAMAD M.Y. MASAUNI (MB.) KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA AFRIKA TAREHE, 3 MACHI, 2026, ZANZIBAR**

***Ndugu Wanahabari,***
***Ndungu Watanzania Wenzangu Mnaotusikiliza kupitia Vyombo vya Habari,***

Awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa siku hii ya leo tukiwa na afya njema.

Tarehe 3 Machi ya Kila mwaka, Bara la Afrika huadhimisha Siku ya Mazingira Afrika. Siku hii adhimu iliasisiwa mwaka 2002 na Baraza la Mawaziri la Umoja wa Afrika ikiwa ni moja ya maazimio muhimu ya Umoja wa Afrika katika kuhimiza nchi wanachama na Bara la Afrika kutunza na kuhifadhi mazingira na rasilimali zake ambazo kwa kiasi kubwa ndio nguzo ya maendeleo na ukuaji wa uchumi, maisha na ustawi wa watu.

Aidha, mwezi Januari 2012, Umoja wa Afrika ulipitisha azimio kwa siku hii pia kuwa siku ya Wangari Maathai '***Wangari Maathai Day"*** kama kumbukumbu ya kutambua mchango wa Profesa Wangari Maathai ambaye alikuwa Kiongozi, mwanazuoni, mwanaharakati wa masuala ya mazingira na Mshindi wa Tuzo ya Nobeli kutoka nchini Kenya ambaye alitoa mchango mkubwa katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira Barani Afrika na katika majukwaa mengine ya Kimataifa.

Kauli mbiu ya siku hii kwa mwaka huu ni ***"Assuring Sustainable Water Availability and Safe Sanitation Systems to Achieve the Goals of Agenda 2063".*** *Ambayo tafsiri yake ni:* ***"Uhakika wa upatikanaji Endelevu wa Maji na Mifumo Salama ya Usafi wa mazingira ili kufikia Malengo ya Ajenda 2063"***

***Ndugu Wanahabari,***
Maendeleo na ukuaji wa taifa lolote duniani pamoja na ustawi wa watu wake vimefungamana na hali na ubora wa mazingira. Hali ya mazingira ikiwa imara ukuaji wa uchumi na ustawi wa watu pia huwa imara.

Mathalani, Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, ilionesha kuwa Tanzania ina watu milioni 61.7, na hivyo kuwa miongoni mwa nchi zenye idadi kubwa ya watu barani Afrika. Vilevile, inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2050 Tanzania inaweza kuwa na watu takriban

milioni 120. Hii inamaanisha kuwa ifikapo mwaka 2050 mahitaji ya rasilimali, makazi, ajira, maji, huduma ya afya, nishati pamoja na huduma za kiikolojia itahitajika kuwa mara mbili ya sasa. Tukumbuke kuwa huduma zote hizo zitakazotakiwa kuwa mara mbili zaidi ya sasa kwa kipindi hicho zitazotokana na ardhi hii hii ya nchi yetu ambayo haitaongezeka hata hatua moja.

Kauli mbiu ya siku ya Mazingira kwa Afrika kwa mwaka huu inayohohusu ***Uhakika wa upatikanaji Endelevu wa Maji na Mifumo Salama ya Usafi wa mazingira kwa maendeleo endelevu*** inatukumbusha umuhimu wa kutekeleza mipango shirikishi ambapo mtu mmoja mmoja, taasisi zetu na wadau wote wa maendeleo ni muhimu kushiriki ipasavyo kwa faida yetu sisi wa Tanzania wa sasa na watanzania wa mwaka 2050 na siku za usoni.

Kwa kutambua uhalisia huu, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kufungamanisha kwa vitendo masuala ya mazingira, mabadiliko ya tabianchi na maendeleo endelevu.

***Ndugu Wanahabari,***
Dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050 imeweka nguzo adhimu inayohusu Uhifadhi wa Mazingira na ustahimilivu dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi. Vile vile, Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeweka masuala ya mazingira na mabadiliko ya Tabianchi kama mojawapo ya masuala muhimu yatakayozingatiwa katika kipindi cha mwaka 2025 – 2030.

Hii ni zaidi ya uthibitisho kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imetoa kipaumbele kwa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kama msingi wa ukuaji wa uchumi na ustawi wa watanzania.

***Ndugu Wanahabari,***
Dunia inapitia katika changamoto kuu tatu za mazingira ambazo ni: Upotevu wa Bioanuai; uchafuzi wa Mazingira kutokana na vyanzo mbalimbali pamoja na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mtakubaliana nami kuwa, rasilimali za mazingira pamoja na changamoto zake hazitambui mipaka ya kiutawala ya milki za nchi, kwa kuwa uchafuzi wa mazingira ukifanyika katika upande mmoja wa dunia unaweza kuathiri upande mwingine wa dunia. Hali kadhalika

samaki wanaopatikana katika bahari au maziwa yetu makubwa hawana uraia wa nchi yoyote kati ya nchi zinazopitiwa na rasimali hizo.

Uhalisia huu unatukumbusha umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kuimarisha uhifadhi wa mazingira pamoja na ufumbuzi wa pamoja wa changamoto za mazingira. Ni kwa muktadha huu, Tanzania ni nchi mwanachaama wa mikataba mbalimbali inayohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira.

***Ndugu Wanahabari,***
Kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano wa Kimataifa katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira, Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na mambo mengine imeimarisha zaidi ushirikiano wa kimataifa na kutoa mchango mkubwa katika masuala ya kikanda na kimataifa yanayohusu mazingira na mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, kupitia ushawishi wa Mheshimwa Rais wetu bkatika medani ya kimataifa, nchi yetu imepata fursa za kuongoza masuala mbalimbali ya kikanda ambayo ni pamoja na:

- Kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika- Misheni 300 uliofanyika tarehe 27 hadi 28 Januari, 2025 jijini Dar es Salaam. Aidha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania ni kinara wa Nishati Safi Afrika na kuhamasisha upatikanaji wa gharama nafuu wa Nishati ya Kupikia Barani Afrika;
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mjumbe wa kudumu wa Kamati ya Umoja wa Afrika ya Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi;
- Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ni Mhandisi Hamad Y. Masauni, ni Makamu Mwenyekiti wa Mkutano wa Nane wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEA - 8) kuanzia Desemba 2025 hadi Desemba 2027
- Uenyekiti wa Kundi la wataalam wa majadiliano ya mabadiliko ya Tabianchi *(African Group of Negotiators, AGN)* kwa kipindi cha mwaka Machi 2025 hadi Januari 2026;
- Uenyekiti na Uenyeji wa Mkutano wa 12 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi uhaohusu Hifadhi ya Mazingira ya Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi utakaofanyika Oktoba, 2026;
- Uongozi wa juu ngazi ya Mkurugenzi Mtendaji katika taasisi ya kikanda chini Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika (LTA) kwa kipindi cha Machi 2026 hadi Machi 2029 ambapo Mkataba huu unajumuisha nchi za Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia.

Vilevile nchi yetu imepata fursa ya kuwa mwenyeji wa:

- Ofisi ya Kikanda ya Mtandao wa Kikanda Kuhusu Kujenga Uwezo wa nchi zinazoendelea kukabiliana na Upotevu na Hasara zitokanazo na Mabadiliko ya Tabianchi *(Regional Office for Santiago Network on Loss and Damage)*;
- Kituo Mahiri cha Kujenga uwezo Vijana kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi *(African Youth Climate Change Centre of Excellence);*

Ni matumaini makubwa ya Mheshimiwa Rais wetu kuwa, Wizara na Taasisi za Umma, Asasi za Kiraia, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, Sekta Binafsi na Watanzania wote tutazitumia fursa hizi katika kuimarisha juhudi za kuhifadhi mazingira na kuongeza ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabinchi nchini; Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya mazingira, mabadiliko ya tabianchi; Fursa za ajira kwa watanzania na fursa za kiuchumi kwa sekta binfasi kupitia taasisi zilizoanzishwa na mikutano itakayofanyika nchini kwetu kupitia shughuli za mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

***Ndugu Wanahabari,***

Nchi yetu imeendelea kuandaa na kutekeleza Sera na nyenzo mbalimbali za kisera kwa lengo la kuimarisha uhifadhi wa mazingira katika sekta zote pamoja na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali zake. Baadhi ya nyenzo hizo ni pamoja na Sera ya Mazingira ya mwaka 2021; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191; Sera na Sheria za Kisekta zinazohusu rasilimali za mazingira kama vile wanyamapori, misitu, mifugo, uvuvi, maji pamoja na sera nyingine zenye mnasaba na mazingira na mabadiliko ya Tabianchi.

Kwa kutumia jukwaa la Siku hii ya Kielelezo ya mazingira ya Afrika, natoa rai kwa wananchi wote wenzangu kuongeza kasi ya kuhifadhi mazingira kwa shughuli mbalimbali ikwemo, Upandaji na utunzaji miti; Udhibiti wa matumizi ya mifuko ya plastiki inayochafua mazingira yetu; kuongeza kasi ya matumizi ya nishati safi ya kupikia; Matumizi bora ya ardhi kwa shughuli mbalimbali za uzalishaji pamoja kuongeza kasi ya utoaji wa elimu ya mazingira kwa umma.

***Ndugu Wanahabari,***

Napenda kuwashukuru wadau wote wa Mazingira na Washirika wa Maendeleo kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ikiwemo, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kutekeleza shughuli na miradi mbalimbali ya kuhifadhi mazingira nchini. Ni matumami yangu kuwa tutaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi ili kukabiliana na changamoto za hifadhi ya mazingira na kuleta maendeleo endelevu nchini.

***Ndugu Wanahabari,***
Kabla sijahitimisha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru vyombo vya habari kwa kutumia muda wenu kuhamasisha jamii kwenye masuala ya hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali zake. Aidha, nizishukuru pia taasisi zote za Serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi na asasi za kimataifa kwa kushirikiana na Serikali kufanya jitihada mbalimbali za kupambana na uharibifu wa mazingira.

***Ndugu Wanahabari,***
Mwisho, natoa wito kwa Mikoa yote kutumia vyombo mbali mbali vya habari vikiwemo, radio za kijamii zilizopo katika Halmashauri zenu kuhamasishana na kuelimisha jamii kwenye masuala yahusuyo hifadhi ya mazingira hususan kutumia nishati mbadala wa mkaa, majiko banifu pamoja na kutumia njia sahihi za kuhifadhi taka. Tukumbuke kwamba, Tanzania yetu ni hii moja hatutakuwa na sehemu nyingine zaidi ya hii, hivyo suala la hifadhi ya mazingira ni jukumu letu sote na tunapaswa kulitekeleza kwa vitendo.

Aidha, nitoe rai kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika juhudi za kuhifadhi mazingira kwa vitendo ikiwemo, kupanda miti, kutunza vyanzo vya maji, kuondokana na matumizi ya plastiki kama vile mifuko ya plastiki, na kuzingatia sheria na kanuni za mazingira.

Maadhimisho ya siku ya mazingira Afrika ni kielelezo na jukwaa adhimu la kutukumbusha wajibu wetu wa kila siku wa kuchukua hatua za makusudi zakutunza na kuhifadhi mazingira yetu pamoja na kuhamasisha maendeleo endelevu nchini. Maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana bila mazingira bora. Kwa kuhitimisha, natoa rai kwenu ndugu wanahabari kuendelea kuwa sauti ya mazingira.

Asanteni kwa kunisikiliza.

*Mha.* Hamad M.Y Masauni (Mb.),
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**
**(MUUNGANO NA MAZINGIRA)**